TAARIFA YA WN-OWM MHE. JENISTA J. MHAGAMA(MB) WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU) KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MCHANGO WA WAKALA KATIKA KUJENGA UCHUMI WA VIWANDA 20 SEPTEMBA 2018 UKUMBI WA LAPF DODOMA.

- **Andrew Masawe, Katibu Mkuu Ofisi ya Wiziri Mkuu, Kazi,Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**
- **Bibi Hadija Mwenda, Kaimu Mtendaji Mkuu wa OSHA;**
- **Viongozi wa OSHA mliopo hapa;**
- **Ndugu Waandishi wa Habari**
- **Mabibi na Mabwana;**

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia afya njema kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo.

Nimeambiwa na Uongozi wa OSHA kuwa baada ya kuongea na mimi mtakaa na Uongozi wa OSHA ili kuwapitisha kwenye shughuli zinazofanywa na Wakala ili mueweze kuzitambua vyema kazi za wakala na hata mtakapokuwa mnawahabarisha wananchi basi muwe na uelewa mpana juu ya kile mnachokiripoti na kuweza kuwaelimisha wananchi. Kubwa zaidi katika kikao hiki ni kusaidia kuwapa wanahabari taarifa ya mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa Taasisi yetu ili kukuza uchumi wa viwanda.

Ndugu Wanahabari

Kama mnavyoelewa Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt.John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasisitiza sana suala la ujenzi wa Uchumi wa Viwanda ili nchi yetu iweze kuzalisha ajira na kuongeza mapato yanayotokana na kodi na mauzo mbalimbali ya bidhaa ndani na nje ya nchi na kufikia uchumi wa pato la kati.

Ili kuunga mkono juhudi za Mh. Rais John Pombe Joseph Magufuli Rais, na katika kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015, Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa kazi (OSHA) imetekeleza na inaendelea kutekeleza, mambo mbalimbali ambayo yatakayosaidia kuendeleza kujenga uchumi wa viwanda hapa nchini.

Bila shaka mnafahamu mtaji namba moja wa Kiwanda ni wafanyakazi, na tunatambua kuwa ili mfanyakazi aweze kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi ni lazima usalama na Afya yake ulindwe. OSHA inaendelea kusimamia suala hilo kwa ukaribu kwa kuhakikisha kuwa sehemu za kazi zinakuwa salama na kuepusha migogoro baina ya Wafanyakazi na Waajiri na kufanya uzalishaji wenye tija. Hata nyie ni mashuhuda kuwa kwa nchi yetu pamoja na kuendelea kupokea wawekezaji wengi maeneo ya kazi yameendelea kusimamiwa ili kuwa

na utulivu na kuhakikisha usimamizi mzuri wa Sheria za kazi ikiwemo sheria ya Afya na Usalama mahali pa kazi unaofanywa na Serikali.

Ndugu Wanahabari,
Nchi yetu kwa sasa inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Miradi hiyo ni kama Ujenzi wa Madaraja ya Juu, upanuzi wa viwanja vya ndege mfano uwanja wa kimataifa Julius Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa (standard gauge), miradi mikubwa ya umeme, mradi mkubwa wa bomba la mafuta, na miradi mingine mingi mikubwa ambayo Serikali ya awamu tano inaendelea kutekeleza. Katika miradi yote hii OSHA imekuwa ikisimamia na inaendelea kusimamia Usalama na Afya kwa wafanyakazi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Matokeo ya usimamizi huu ni kwamba umepelekea kupunguza ajali na magonjwa, migogoro kazini, kupunguza gharama za utekelezaji na hivyo kufanya miradi hiyo kukamilika katika viwango vilivyokusudiwa na kumalizika kwa wakati.

Ndugu Wanahabari,
Kwa mwaka wa fedha 2017/18 jumla ya ajali 755 ziliripotiwa kwa mujibu wa Sheria, ambapo 6 kati ya hizo zilisababisha vifo, 749 majeruhi. Aidha, Sekta ya Uzalishaji iliongoza kwa kuwa na asilimia 87 ya ajali zote ambapo sekta ya madini ilikuwa na asilimia 7, ujenzi asilimia 4 sekta zilizobaki asilimia 2.

Ndugu Wanahabari,
Aidha, ikumbukwe kuwa kujenga uchumi wa viwanda, kutaambatana na kuingiza teknolojia mpya zitakazoambatana na vihatarishi vya kiafya na usalama.
Sheria ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi Na. 5 ya Mwaka 2003 ilikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa inaweka utaratibu wa kulinda Afya na usalama wa Wafanyakazi wawapo sehemu za kazi na kuhakikisha kuwa kunakuwa na kinga dhidi ya vihatarishi kwa Afya na Usalama ili kuhakikisha kuwa sehemu ya kazi panakuwa mahali salama kwa kila mtu.

Sheria hii ililenga kutekeleza mkataba wa kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Na. 155 wa mwaka 1981 kuhusu masuala ya Afya na Usalama mahali pa kazi.

Ndugu Wanahabari,

Mwezi Machi, 2018 Mhe. Rais kwa utaratibu wake mzuri alikutana na Wadau kutoka Sekta Binafsi ikiwa ni pamoja na TPSF ili kuzungumzia namna ya kujenga mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini na kuongeza kasi ya uwekezaji hasa katika viwnada na vilevile kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kushiriki katika miradi ya ujenzi wa uchumi nchini,pamoja na mambo mengi yaliyojadiliwa na kuazimiwa ilikuwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Sheria ya Afya na Usalama mahala pa Kazi Na. 5 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake ili bila kuondoa wajibu wa OSHA katika kulinda afya za wafanyakazi bali kuona namna ya kupunguza baadhi ya Tozo za kikanuni na kupunguza mzigo wa uendeshaji katika uwekezaji nchini. Katika kutekeleza jambo hilo OSHA imefanya mambo yafuatayo:-

1. Kutengeneza program maalum ya utoaji Elimu kwa wadau kuhusu takwa la kisheria la kulinda afya za wafanyakazi nchini mahala pa kazi katika Kanda mbalimbali.

2. Kuondoa baadhi ya Ada na tozo zisizoondoa wajibu wa muajiri kulinda Afya za Wafanyakazi mbali zinazoondoa mzigo wa mwekezaji katika kuwekeza kwenye uchumi hasa uchumi wa viwanda.

3. Kusimamia mifumo ya utendaji wa watumishi wa OSHA ili kuondoa mianya ya rushwa na kukuza uzalendo na uwajibikaji.

Tozo zilizoondolewa au kufanyiwa marekebisho ni pamoja na:-

Na		**Mwanzo**	**Sasa**	**Sababu**
1.	Kufuta ada ya Fomu ya Usajili	Tsh. 2,000	Imefutwa	Kupunguza gharama.
2.	Kufuta ada ya Usajili wa maeneo ya kazi kwa kuzingatia ukubwa wa eneo.	(iliyokuwa ikitozwa Tshs 50,000 hadi Tshs 1,800,000 kulingana na eneo la kazi),	Imefutwa.	Kuboresha mazingira ya biashara.
3.	Kufuta faini inayohusiana na vifaa vya kuzimia moto	Tshs. 500,000	Imefutwa Kuondoa *Double payment*	Kupunguza gharama za uendeshaji.
4.	Kufuta ada ya Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi	iliyokuwa ikitozwa Tshs 200,000 kwa mwaka)	Imefutwa	Kuboresha mazingira ya biashara.
5.	Kufuta Tozo ya siku ya Ushauri wa kitaalamu wa Usalama na Afya kwa kuzingatia idadi ya wafanyakazi.	Tshs 450,000	Imefutwa	Kupunguza gharama ili kutoa elimu kwa wahitaji wengi zaidi.

Ndugu Wanahabari,

Jambo lingine ambalo nilitaka mlifahamu ni kuwa, kumekuwa na dhana ya kuwa utekelezaji wa Sheria ya afya na usalama mahali pa kazi unaihusu Sekta binafsi tu, lakini ukweli ni kwamba sheria hii ina husu pia Sekta ya Umma. na kesho tumewaita wakuu wote wa Taasisi na Wakurugenzi wa Rasilimali watu na Wakurugenzi wa Mipango kutoka Wizara zote kuja kujadili namna bora ya utekelezaji wa sheria hii katika Sekta ya Umma.

Aidha, utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Usalama Mahali pa Kazi, namba 5 ya mwaka 2003 utasaidia kuongeza ufanisi na tija kwa watumishi wa umma, vilevile utapunguza gharama za matibabu ambazo zinazotolewa na serikali kupitia mfuko wa bima ya afya kwa

wafanyakazi na mfuko wa fidia kwa wanyakazi. Na hili litafanya mifuko hii kuwa endelevu.

Ndugu wanahabari,
Msisitizo huu pia ni matakwa ya malengo ya Umoja wa Mataifa na utekelezaji wa vipengele vilivyomo kwenye Lengo namba nane (8) la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo ni kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wote ifikapo mwaka 2030 pamoja na kukomesha ajira mbaya za watoto ifikapo mwaka 2025.

Ndugu waandishi wa Habari,Baada ya maelezo haya mafupi naomba kuwasilisha.

Jenista J. Mhagama (Mb)
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU
(SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU)